# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MWONGOZO WA MAKISATU-2020

## 1.0 UTANGULIZI

Mnamo tarehe 5 Desemba 2016, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako (Mb), wakati akifungua Mashindano ya Ujuzi kwa ukanda wa Afrika Mashariki ambayo yalifanyika Jijini Dar es Salaam, katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Mhe. Waziri aliwaagiza Wakuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), kuandaa tukio la Kitaifa la Mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

Katika kutekeleza agizo hilo, Wizara ikishiriana na COSTECH, DIT na VETA, ilifanya Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU-2019). Kilele cha MAKISATU kilifanyika Jijini Dodoma kuanzia tarehe 5-7 Machi, 2019. Mashindano hayo yalijumuisha wabunifu kutoka makundi sita tofauti ikiwemo, Wanafunzi wa Sekondari; Ufundi Stadi; Sekta isiyo Rasmi; Ufundi wa kati; Utafiti na Maendeleo; na Vyuo Vikuu. Mashindano haya yalikuwa na kaulimbiu ya "**Kukuza Ujuzi na Ubunifu kwa Uchumi wa Viwanda**". Mafanikio yaliyopatikana katika mashindano hayo ni kutambua wabunifu mahiri 60 ambao taratibu za kuwaendeleza kufikia ubiasharishaji wa bunifu zao unaendelea kati ya jumla ya wabunifu 407 walioshiriki kuanzia hatua za awali. Wizara inapenda kuujulisha umma wa Watanzania kuwa MAKISATU yatakuwa yakifanyika kila mwaka kulingana na kalenda itakayotolewa kwa mwaka husika.

## 2.0 LENGO LA MASHINDANO

Lengo la mashindano haya litakuwa ni kutambua na kuendeleza ubunifu kwa kuhakikisha ubunifu unaotambuliwa unaendelezwa na kubiasharishwa ili kusaidia katika kuifanya Tanzania kuwa na uchumi wa kati unaotengemea viwanda vya ndani.

## 3.0 MAKUNDI YA WABUNIFU NA MFUMO WA UPATIKANAJI KATIKA MAKISATU 2020

Mashindano haya yatashirikisha makundi saba na wabunifu watatoka katika mikoa yote Tanzania. Makundi hayo yatakuwa ni Shule za Msingi (Serikali na Binafsi); Shule za Sekondari (Serikali na Binafsi); Vyuo vya Ufundi Stadi; Sekta isiyo Rasmi; Vyuo vya Ufundi wa kati; Taasisi za Utafiti na Maendeleo; na Vyuo Vikuu.
Mwisho wa mchakato wa kutambua wabunifu kila kundi litashirikisha wabunifu mahiri kumi (10) katika fainali za Mashindano. Mchakato wa kuwapata wabunifu utaratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) ikishiriana na COSTECH, DIT na VETA.

Upatikanaji wa wabunifu katika kundi la Shule za Msingi; na Shule za Sekondari utaratibiwa na WyEST ikishirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia kwa Makatibu Tawala wa Mikoa yote Tanzania Bara. Kila mkoa utawasilisha majina matatu (3) ya wabunifu Mahiri kutoka kila kundi yaani kundi la Shule za Msingi na Shule za Sekondari katika Mkoa husika. Baada ya mawasilisho hayo mashindano ya nusu fainali kwa kundi la wanafunzi yatafanyika Kitaifa kupata wabunifu mahiri kumi (10) kwa kila kundi watakaoshiriki katika fainali za kitaifa zitakazojumuisha makundi yote.

Upatikanaji wa wabunifu wa Kundi la Vyuo vya Ufundi Standi na Sekta isiyo Rasmi; utaratibiwa na VETA kwa kuwasilisha maombi kulingana na maelekezo yatakayotolewa kwa kundi ambalo mbunifu anatokea. Kisha Mamlaka itafanyia tathmini maombi yaliyowasilishwa na kupata wabunifu mahiri kumi (10) kutoka kila kundi ambao watashiriki katika fainali za kitaifa.

Upatikanaji wa wabunifu wa Kundi la Vyuo vya Ufundi wa kati utaratibiwa na DIT ambapo wabunifu watawasilisha maombi yao kulingana na maelekezo yatakayotolewa. Kisha baada ya mawasilisho Taasisi itafanyia tathmini ya mawasilisho yote na kupata wabunifu mahiri kumi (10) watakaoshiriki kwenye fainali za kitaifa.

Upatikanaji wa wabunifu wa makundi ya taasisi za Utafiti na Maendeleo; na Vyuo Vikuu utaratibiwa na COSTECH, Maombi ya wabunifu yatawasilishwa katika Tume kulingana na maelekezo yatakayotolewa. Baada ya mawasilisho ya maombi COSTECH watafanyia tathmini ya mawasilisho katika kundi husika na kupata wabunifu mahiri kumi (10) kwa kila kundi ambao watashirika katika fainali za kitaifa.

Aidha, mawasilisho yote ya wabunifu yatafanyika kwa kutumia fomu WTF 7 pamoja na maelekezo ya tathmini yanayopatikana katika fomu WTF 8 zinazopatikana katika Mwongozo wa Kitaifa wa Kutambua na Kuendeleza Ugunduzi, Ubunifu na Maarifa Asilia-2018.

## 4.0 KANUNI ZA USHIRIKI KATIKA MAKISATU

(a) Mgunduzi/Mbunifu/Mmiliki wa Maarifa Asilia ni lazima awe Mtanzania, hapa hakuna kiwango cha umri wala elimu kwa mshiriki;

(b) Ubunifu unaowasilishwa katika Mashindano uwe ni mali ya mbunifu mwenyewe na si vinginevyo;

(c) Ubunifu wake uwe haujawahi kushirikishwa katika fainali za kitaifa za MAKISATU za miaka iliyopita;

(d) Kwa Ubunifu uliowasilishwa katika hatua za awali kwenye mchakato wa kupata wabunifu kwenye makundi na ukashindwa kuchaguliwa kushiriki katika fainali za kitaifa, unaweza kuwasilishwa ukiwa na maboresho;

(e) Kwa ubunifu unaofanywa na vikundi au taasisi, wakati wa kuwasilisha maombi uwasilishwe kwa Jina la taasisi au kama ni kundi la wabunifu kwa Jina la kikundi au Jina la kiongozi katika ubunifu huo na sio wabunifu wote;

(f) Katika Fainali za Mashindano ya MAKISATU 2020 kila ubunifu utawasilishwa na mbunifu mmoja, na endapo kutakuwa na ugharamiwaji mbunifu mmoja tu kwa kila ubunifu atagharamiwa na sio kikundi cha wabunifu;

(g) Mgunduzi/Mbunifu anaruhusiwa kuwasilisha ubunifu zaidi ya mmoja katika hatua za awali za makundi bila kipangamizi;

(h) Ikitokea mbunifu hana uwezo wa kujaza fomu ambayo atatakiwa kuijaza msaada wa kujaziwa fomu utatolewa na waratibu wa mashindano waliopo karibu nae kwa mahojiano ya ana kwa ana au kwa njia ya simu; na

(i) Wakati wote wa mashindano mshiriki/mbunifu atatakiwa kufuata maelekezo na miongozo itakayokuwa inatolewa na waratibu kwa kadiri mchakato wa mashindano utakavyokuwa ukiendelea na kufuatilia kalenda ya mashindano.

## 5.0 UTARATIBU WA MAKISATU

(a) Kamati ya maandalizi itatoa matangazo ya kuhamasisha ushiriki wa wabunifu katika mashindano;

(b) Wabunifu watawasilisha maombi ya ushiriki kupitia kwa waratibu wa kundi husika kama yalivyoanishwa hapo juu, mawasilisho yatafanyika kwa kupitia fomu maalum zilitajwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa kutambua na kuendeleza ugunduzi, ubunifu na maarifa asilia na kwa kupitia tovuti ya mashindano ya www.makisatu.costech.or.tz kwa kipindi maalum kitakachotangazwa;

(c) Waratibu wa kila kundi watafanya tathmini ya mawasilisho ya kundi na kuchagua ubunifu bora kumi (10) kwa kila kundi ambazo zitashiriki katika fainali ya kitaifa, **isipokuwa** kwa makundi ya wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari kutafanyika nusu fainali ya kitaifa ili kupata wabunifu bora kumi (10) watakaoshiriki katika fainali za kitaifa kwa kila kundi;

(d) Kamati ya maandalizi itaandaa mashindano na maonesho ya kitaifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu ambapo ubunifu ulioshinda katika ngazi za makundi utaoneshwa na kushindanishwa;

(e) Timu ya wataalamu (majaji) itafanya tathmini ya kina kwa kila ubunifu ikiwa ni pamoja na kupokea maelezo kutoka kwa mbunifu mwenyewe, kisha ulinganifu wa alama zilizopatikana utafanyika na kupata washindi mahiri watatu (3) kwa kila kundi watazawadiwa na kupewa tuzo mbalimbali;

(f) Wizara itatoa vyeti vya ushiriki kwa washiriki na washindi wote; na

(g) ubunifu utakaokuwa umeshiriki katika hatua ya fainali utaingizwa katika mpango wa kuendelezwa ili kuweza kubiasharishwa kutokana na uhitaji utakao ainishwa na baada ya tathmini za kitaalamu.

## 6.0 UTARATIBU WA KUWAENDELEZA WABUNIFU

Uratibu wa kuendeleza wabunifu baada ya kutambuliwa kupitia mashindano haya utaratibiwa na COSTECH. Uratibu huo utafuata sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya serikali kama inavyonesha hapo chini.

## FOMU YA MAOMBI YA TUZO (WTF 7)

---

## MAOMBI YA USHIRIKI KATIKA MASHINDANO YA KITAIFA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU (MAKISATU)

1. Tafadhali jaza taarifa na anwani yako

(a) Jina………………………………………………………………………………………..……

(b) Anwani ………………………………………………………………………………………...

(c) Simu……………………………………………………………..…………………………...

(d) Taasisi unayotoka ……………………………………………………………………………

(e) Makazi……………………………………………………………..………………………..………

(f) Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………..……………...

(g) Barua pepe………………………………………………………………………………..………

(h) Uraia …………………………………………………………………………………………...

(i) Kiwango cha Elimu…………………………………………………………………………….

(j) Taaluma………………………………………………………………………………………...

(k) Kazi ……………………………………………………………………………………………

2. Maombi yanahusu (weka alama ya √ panapohusika)

a. Ugunduzi (teknolojia mpya iliyogunduliwa kwa mara ya kwanza ambayo haijawahi kuwepo) …………………..
b. Ubunifu (teknolojia iliyoboreshwa kutoka kwenye zile zilizopo) ………………………..
c. Matumizi ya teknolojia katika mazingira mapya …………………………...

3. Jina la Ugunduzi/ubunifu: ……………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..................

4. Muhtasari kwa ufupi wa maombi yako ………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

5. Je, ugunduzi/ubunifu wako unatatua tatizo gani la kiufundi ?

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………….

6. Kutokana na tatizo uliloainisha hapo juu, je ni ufumbuzi gani wa kiufundi ambao ugunduzi/ubunifu wako unatatua ? (Elezea kwa undani, ikiwa ni pamoja na maelezo yanayohusu michoro muhimu, picha na maelezo mengine).

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

7. Toa maelezo yanayohusu kazi ambayo imekwishafanyika katika eneo lako la ubunifu/ugunduzi.

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

8. Je, ni kitu gani kipya unachodai katika ugunduzi wako ukilinganisha na vile ambavyo vilishafanyika? Toa maelezo ikiwa unafahamu kama ugunduzi wako umewahi kufanywa na mtu mwingine.

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………

9. Toa maelezo ya umuhimu wa ugunduzi wako:

a) Jinsi ulivyochangia au unavyoweza kuchangia kujenga maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi hapa nchini ……………………………………………………………………………………………………….
………………………………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………………………….

b) Jinsi ulivyochangia au unavyoweza kuchangia katika kujenga au kuendeleza taaluma?
………………………………………………………………………………………...………………………
………………………………………………………………………….………………………………..

c) Jinsi gani umewekwa au unaweza kuwekwa kwenye matumizi ya kuboreshs maisha ya wananchi?
……………………………………………………………………………………………...…………………
…………………………………………………………………………….…………………………..

10. Je, ubunifu/ugunduzi wako umekamilika tayari katika kiwango cha kutumika?

Ndiyo/Hapana (Kata isiyohusika)

Kama ndiyo, elezea kwa ufupi.

……………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………….…………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………….

11. Je kuna mtu mwingine ambaye ameshiriki katika ubunifu/ugunduzi huo?

Ndiyo/Hapana (Kata isiyohusika)

Kama ndiyo, elezea kwa ufupi.

……………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………….…………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………….

12. Jinsi gani umepata taarifa juu ya mashindano haya.

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………….…………………………………………………………...

13. Je, una ulemavu wa aina yeyote? Ndiyo/Hapana (Kata isiyohusika), Kama ndiyo, taja aina ya ulemavu.

………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………….……………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………….

Maombi haya pamoja na taarifa zingine zitumwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA),
S.L.P. 2849,
**Dar es Salaam**
Email: pr@veta.go.tz au info@veta.go.tz

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 31 Januari 2020.

Unaweza kupata ufafanuzi zaidi kwa kupiga 0652226688/0712148332